# KISWAHILI.
# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KIDATO CHA TATU 2026
# MWISHO WA MUHULA WA PILI

1. UFAHAMU

a) Wagonjwa wanaoendelea kuangamia kutokana na ugonjwa huu wanaendelea kufikia kiwango cha kutisha. 1x1

b) Maradhi haya hayasabibishi uchungu wowote mwanzoni.
1x2

c) i) Mahusiano ya kimapenzi katika umri mdongo.
ii) Uwepo wa mahusiano wa kimapenzi na wengi.
iii) Matumizi ya dawa Fulani za kupanga uzazi.
iv) Uvutaji wa sigara. zozote 3 x 1= 3

d) i) Ukaguzi wa kibinafsi wa mara kwa mara wa viungo vyenye uwezekano mkubwa wa kuambukizwa.
ii) Kumwona daktari iwapo pana uvimbe kwenye viungo au ugumu wa kumeza. 2x1=2

e) i) Ulaji wa vyakula vinavyosheheniwa na protini k.v. nyama na mayai.
ii) Mitindo ya kisasa ya maisha k.v matumizi ya vipodozi vyenye zebaki.
iii) uvutaji sigara
iv) unywaji pombe 2x1=2

f) Tafiti zinazoendelea kufanywa kutafuta tiba ya saratani zimeanza kuzalisha matunda na pana matumaini kuwa tiba faafu itapatikana.
1x2=2

g) i) Maradhi sugu
ii) Matiti
iii) Uchunguzi wa mara kwa mara. 3x1=3

2. UFUPISHO

A

- Maarifa huyadhibiti maisha ya binadamu
- Anayekosa maarifa huathirika pakubwa
- Maarifa ni utajiri anaotumia binadamu kujifaidisha
- Elimu ni chimbuko la maarifa
- Maarifa yenyewe haina upinzani
- Kila mtu ana uhuru wa kutumia maarifa kukuza maarifa mengine
- Utumiaji wa maarifa hauyamalizi maarifa
- Maarifa hayagusiki ( alama 5 ,mtiririko 1)

B

- Maarifa huingiliana na maarifa mengine
- Maarifa yanaweza kuhamishwa
- Maarifa yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya ishara au mitindo mingine
- Yanawezwa kubadilishwa au kugeuzwa ili kuwasilishwa kwa njia nyepesi
- Yana sifa ya uhusianaji
- Huweza kuhifadhiwa katika nafasi ndogo
- Hayawezi kudhibitiwa au kuzuiliwa yasambae
- Yanaenea haraka
- Huepuka pingu za watu (alama 8,mtiririko 1)

  Maarifa ni nguvu inayoshinda nguvu zote



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

## MATUMIZI YA LUGHA

a) i) /k/
ii) /ny/
iii) /z/ 3 x 1 = 3)

b) M – mi – mkono – mikono
Mw- mi – mwiko – miiko
Mu – mi- muwa- miwa 2 x 1 = 2

c) angali – kitenzi kushirikishi kikamilifu(t)
angali – kitenzi kisaidizi (Ts)
anaendesha – kitenzi kikuu (T)
imechakaa – kitenzi halisi (T)

4 X½ = 2

d) a – nafsi ya tatu umoja/ngeli
f – mzizi wa neno
a – kiishio
ye – kirejeshi

4 X ½ = 2)

e) ta – ujao } wakati ujao hali timilifu
me – timilifu

2 x½ = 1

f) kwa - kiulizi
kwao – mahali
kwa – muda

g) safiri – safirishika,
badili – badilishika
starehe- starehesheka

1 x 1 = 1)

h)i)Kemunto anawa mkono wake baada ya kugusa majani ya kiwavi. (majani)
ii)Shingo iliniwasha baada ya kutambaliwa na mdudu aitwaye kiwavi.

2 x 1 = 2)

i) Mtihani, mtahini, mtahiniwa, utahini, kutahini 2 x 1= 2

j) S → KN + KT
KN → S
S → Kikulacho
KT → t + E + E
t → ni
E → nguoni
E → mwako 8

x½ = 4)

k) Simu tamba imenirahisishia mawasiliano. (kishazi huru)
ambayo ameninunulia – kishazi tegemezi

2 x 1 = 2

l) Akifika mapema atampata. 1 x 2 = 2



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

m) mzigo – kipozi
mjomba – kitondo
baiskeli – ala
3 x 1 = 3)

n)i) *Mama sokoni ataenda asubuhi kesho. (kinyota)
ii) Gazeti la Taifa Leo huandikwa kwa Kiswahili. (Mstari)
Au
'Gazeti la Taifa Leo' huandikwa kwa Kiswahili. (mtajo)

2 x 1 = 2)

o) ''Watu wanaopenda kukaa bwerere huishia kuwa wezi wa mababu.'' Chifu alituambia.

(3x 1=3)

p) Jizi hili halikuiba jisu na gombe la janajike lile.
6 x½ = 3)

q) i) Walipewa soda pamoja na chupa.
ii) Walipewa soda ikiwa ndani ya chupa.
1 x 2 = 2)

r) i) Shinda
ii) Zidi
iii) Pita
iv) Weza

1 x 1 = 1

**ISIMU JAMII**

a) – Kuwepo kwa lahaja nyingi – baadhi yazo hazingeeleweka na kila mtu.
- Kulikuwa na haja ya kuwa na hati sawa ya kuandika Kiswahili.
- Kulikuwa na haja ya kusawazisha maandishi ya kitaalamu katika kamusi.
- Haja ya kuwa na lugha moja ya mawasiliano na elimu kutumika katika kamusi.
- Haja ya kuwa na lugha moja ya kutumika katika mikutano, shuleni, vyuoni.

5 x 1 =5)

b) Sajili ya mazishi/ matanga/ kilio masikitiko/ msiba/ maombolezo/ uzikaji

(1 x 1= 1)

Sifa
- Msamiati maalum- makiwa marehemu.
- Lugha ya kufarihi/liwaza.
- Yenye matumaini.
- Matumizi ya vihisishi.Oh, Wuui.
- Lugha ya kusitasita.
- Huhusisha mambo ya kidini na mungu na imani ya jamii.
- Kuchanganya ndimi
- Huandamana na viziada lugha
- Matumizi ya sentensi fupifupi.
- Lugha isiyozingatia kanuni za kisarufi.

▪ (zozote 4 x 1 = 4)


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

## FASIHI SIMULIZI

**a) Jukumu la kudumisha fasihi simulizi**

-kufanya F.S kuwa hai kiutendaji kupitia sherehe tofauti za kiserikali.
- Kuhifadhi tanzu mbalimabli ili vizazi vijavyo viweze kuzifahamu mfano kwa kurekodi.
- Kufanya utafiti wa kina kuhusiana na tanzu za F.S.
-Kuhakikisha kuwa lugha za kiasili hizififii kwa vile ndizo chanzo cha fasihi simulizi.
-Kuonyeshwa kwa fani mbalimbali za fasihi simulizi kwenye vyombo vya habari kama runinga.
-kuhimiza wanajamii hususan viongozi kuwasilisha ujumbe wao kwa kutumia fani za fasihi simulizi kwa mafano hotuba,ulumbi,mawaidha n.k.

(6 x 1 = 6)

**b) Udhaifu wa miviga.**

i) Huhatarisha maisha – Baadhi ya miviga kama kutia wasichana unyagoni na kurithi mke wa mtu huhatarisha maisha ya wanajamii na pia zimepitwa na wakati.
ii) Hukinza malengo ya kitaifa – Baaadhi ya miviga kama kutia unyagoni kwa lazima na ukeketwaji wa watoto wa kike ni ukuikaji wa haki za binadamu.
iii) Hujaza hofu – Miviga inayohitaji kafara ya binadamu katika baadhi ya jamii na zile za kufukuza pepo huogofya.
iv) Huhusisha ushirikina – Mazishi katika baadhi ya jamii huandamana na ushirikina ambao huweza kusababisha uhasama baina ya koo.
v) Ni ghali–Baadhi ya sherehe za miviga hugharimu kiasi kikubwa cha pesa/mali na kuiacha jamii katika hali duni kiuchumi,mfano,shereheza kuomboleza.

(5 x 1 = 5)

**c)Aina za miviga katika jamii ya kisasa.**

i) Arusi/ndoa
ii) Mazishi
iii) Kutawazwa kwa viongozi
iv) Kuhitimu kwa wanajeshi
v) Kumpa mtoto jina

(4 x 1 = 4)

**d) Nafasi ya miviga katika jamii**

i ) Huelimisha – mfano katika jando vijana huelimishwa kuhusu mambo yanayohusu utu uzima.
ii) Ni kitambulisho cha jamii – kila jamii huwa na miviga yake mahususi.
iii) Huonyesha matarajio ya jamii kwa vijana/wanajamii.
iv) Huhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii,hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
v) Hukuza uzalendo – huwahimiza wanajamii kuzionea fahari tamaduni za jami izao.
vi) Hukuza na kuhimiza umoja miongoni mwa wanajamii.
vii) Huonyesha Imani za kidini za jamii.

Zozote tano Hakiki majibu ya wanafunzi.

(5 x 1 = 5)



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes